# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL MOCK 2017
# KISWAHILI PAPER 3

## SEHEMU A - SWALI LA LAZIMA

**MSTAHIKI MEYA na Timothy M. Arege**

1. Nanyi vilevile msikate tamaa. Endeleeni kushinikiza kumwona...mlango hatimaye huenda ukasalimu amri...

   a) Eleza muktadha wa nukuu (Al 4)

   b) Eleza mbinu mbili za lugha kutoka kwa nukuu (Al 2)

   c) Eleza sifa nne za anayezungumza (Al 4)

   d) Mlango ungesalimu amri wangefaidi nini, fafanua (Al 10)

## SEHEMU B - RIWAYA

**KIDAGAA KIMEMWOZEA na Ken Walibora**

2. Ni kesi ngapi alizoamua...kwa upendeleo na udhalimu wake? …neno lake lilikuwa ndilo sheria na asemalo ndilo liwalo...moyoni waliwashwa na tashtiti alizowafanyia kila uchao.

   a) Eleza muktadha wa nukuu hii (Al.4)

   b) Eleza mbinu mbili za lugha katika nukuu (Al 2)

   c) Moyoni waliwashwa na tashtiti alizowafanyia kila uchao, fafanua (Al 12)

3. Amani na Imani ni kielelezo chema kwa vijana kwa jinsi wanavyoweza kuitetea na kuikomboa jamii kutokana na dhuluma na tawala za kiimla, jadili haya kwa kuwarejelea wahusika hawa. (Al 20)

## SEHEMU C - MASHAIRI

4. ***Soma Shairi hili kisha ujibu maswali***

Bisimilahi naanza, kuandika na kupima
Wasome watu wa Mwanza, mambo Leo kuwa wema
Sina haja kulibanza, lisomwe na wote umma
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi

Hivi leo naeleza, mama wa kambo si mama
Visa vyake vyauguza nashindwa hata kusema
Ya haki atapuuza, akakulie zahama
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Ubaya atakujaza, aseme huna heshima
Usemalo atazoza, kwa sauti kulalama
Ya haki atayabeza, sheria atenge nyuma
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Mama wakambo aweza, kukufanyia hikima
Kilo chake kupoteza, aseme kaiba Jumia
Niliweka penye meza, amekitwaa Salima
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Uovu akishakoza, na nyumba ataihama
Mzee akufukuza, hanayo tena huruma
Maneno utamaliza, mbele mama kasimama
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Hapo mama akataza, akuzidishe kilema
Apite akitangaza, huyu si mwana ni nyama
Eti anipeleleza, anifata nyuma nyuma
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi

Haishi kunichokoza, hunifanyia tuhuma
Huthubutu kuniweza, mimi ni mtu mzima
Hatoweza kunichuza, kinda la bibi Mwajuma
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Namshukuru Muweza, moyoni yanisakama
Kwa haya ya miujiza, aliyenitenda mama
Machungu ninayameza, namkabidhi karima
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Inshallah yatutokeza, ijapo mwaka mzima
Kweli ikishachomoza, muongo hurudi nyuma
Hana budi kupooza, akae ashike tama
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Atajuta na kuwaza, kidole atajiuma
Watoto nitawakuza, kwa ugonjwa na uzima
Jaribu kunisikiza, kwa hii yangu kalima
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Maneno yanatatiza, mume mate anatema
Usiku uie wa kiza, umenitoka mapema
Majibu yanateleza, nikifikiri yachoma
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

Kwa heri Bibi Aziza, rudi kwenu kwa salama
Umenijazia jazia, watoto kuwasukuma
Wauma akipuliza, na huku wanila nyama
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

*Good-bye* Kiingereza, kwa herini wanachama
Kutunga nimemaliza, na sasa na kaditama
Maneno nimebakiza, nangoja mtu kurama
Mama wa kambo si mama, iliyobaki ni basi.

**Maswali:**

1. Eleza dhamira ya shairi hili (alama 4)
2. Kwa kuzingatia vina na vipande, eleza bahari mbili za shairi hili (alama 2)
3. Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)
4. Eleza toni ya shairi (alama 2)
5. Andika ubeti wa 12 kwa lugha tutumbi. (alama 4)
6. Fafanua msamiati ufuatao kwa mujibu wa shairi. (alama 3)
   a) Wauma ukipuliza
   b) Moyoni yanisakama
   c)Yatayabeza



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

5. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

1. Sie watu weusi, upataje weusi?
2. Kila kitu kibaya, hupewa sifa mbaya
3. Sifa hii 'eusi', yaleta wasiwasi
4. Rangi hii hakika, ni wapi ilitoka?
5. Ibada ya weusi, harusi kuzitusi
6. Kama mtu mweusi, Lusifa ni mweusi
7. Ibada ya weupe, hupokewa peupe
8. Adamu naye Hawa, weupe walipewa
9. Yesu mwana wa Mungu, alikuwa mzungu
10. Malaika wa Mungu, daima walikuwa wazungu
11. Mweusi ti hatendi, silaumiwe purdi
12. Mweusi duniani, likosa kitu gani?
13. Mweusi umeiga, hata ya kutoiga
14. Asojali mkuu, atavunja guu
15. Baa mejitakia, nani takulilia?

**Maswali**

1. Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu (alama 1)
2. Eleza umbo la shairi hili (alama 4)
3. Eleza maudhui ya shairi hili (alama 4)
4. Fafanua mbinu alizotumia mshairi ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (alama 4)
5. Ni nini dhamira ya mtunzi (alama 2)



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

6. Taja na ueleze umuhimu wa mbinu ya uandishi inayotawala katika shairi zima (alama 2)
7. Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa kwenye shairi (alama 2)

(i) Mweusi umeiga, hata ya kutoiga

(ii) Baa mejitakia, nani takulilia?

## SEHEMU D - HADITHI FUPI

**6.** **MWANA WA DARUBINI** - Christine Mwende Mbai

a) Eleza ufaafu wa anwani ya Mwana wa Darubini kwa kufafanua hoja tano.(Al. 10)

b) Maudhui ya usiri yameangaziwa kwa kina katika hadithi hii.Huku ukitoa hoja tano toshelevu,thibitisha. (Al. 10)

7. **GILASI YA MWISHO MAKABURINI** - Said A.Mohamed

"Na wewe sharti unigande mimi kama kupe?"

a) Eleza muktadha wa dondoo. (Al. 4)

b) Eleza mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika nukuu. (Al. 4)

c) Eleza sifa za anayezungumza. (Al. 4)

d) Ni yepi yanayotokea baada ya mazungumzo. (Al. 8)

## SEHEMU E - FASIHI SIMULIZI

8. a) Fafanua vijipera hivi vya fasihi simulizi. (Al. 8)

i) Misimu
ii) Mighani
iii) Wawe/vave
iv) Nyiso

b) Eleza sifa nne za mivigha. (Al. 4)

c) Eleza mbinu ambazo mtambaji wa hadithi atazitumia ili kuteka hisia za hadhira yake. (Al. 8)



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com